

-MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)



**MKATABA WA KAZI YA KUWEKA UMEME UJENZI WA CHUO CHA VETA
MKINGA**

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 09 mwezi 03 2022

KATI YA

Mkurugenzi wa Kanda, VETA Kanda ya Kaskazini, S.L.P. 1738, Moshi, ambaye anaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802, Dodoma (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

Laurent M. Tairo wa TANGA (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundu") kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mwajiri anajenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mkinga;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mkinga;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundu kwa ajili ya kazi ya kuweka umeme ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mkinga;

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundu nakala ya michoro pamoja na mchanganuo wa kazi za Ujenzi vinavyoonyesha kazi zitakazofanyika.

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO;

1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, gharama za ufundi ni Shilingi za Tanzania 25,639,000.00 (Milioni Ishirini na tano laki sita na elfu thelathini na tisa tu.)

Fundi atafanya kazi ya kuweka umeme majengo kumi na saba (17) kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

